# STD 4 MID TERM 3 EXAM 2019

# KISWAHILI

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.*

___1___saa kumi na mbili za___2___, upepo mkali ulianza kuvuma. Upepo___3___ulivuma kwa muda wa ___4___thelathini; kisha kibaridi___5___kuingia. Mwendo wa saa moja kamili mvua___6___ikamwagika kutoka angani. Mvua hii ikafuatwa___7___ngurumo na radi. Mara stima zikapotea na giza___8___likatanda. Baada ya muda mfupi stima zikarejea.___9___ya watoto kumaliza kushangilia kurejea kwa stima, zikapotea___10___. Mara hii zikapotea___11___. Ilibidi tuwashe mishumaa___12___kuitumia kwa shughuli___13___kabla ya kwenda kulala. Mvua___14___kunyesha hadi asubuhi. Msimu wa___15___ulikuwa umeanza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **A.** kilipofika | **B.** kulipofika | **C.** ilipofika | **D.** kulipovika |
| 2. | **A.** asubuhi | **B.** jioni | **C.** mchana | **D.** alfajiri |
| 3. | **A.** hii | **B.** hiki | **C.** hili | **D.** huu |
| 4. | **A.** dakika | **B.** siku | **C.** sekunde | **D.** miezi |
| 5. | **A.** ikaanza | **B.** kikaanza | **C.** akaanza | **D.** likaanza |
| 6. | **A.** mkubwa | **B.** kikubwa | **C.** kubwa | **D.** jikubwa |
| 7. | **A.** wala | **B.** lakini | **C.** bali | **D.** na |
| 8. | **A.** totoro | **B.** ndi | **C.** tititi | **D.** pipipi |
| 9. | **A.** Mbele ya | **B.** Kando ya | **C.** Kabla ya | **D.** Juu ya |
| 10. | **A.** pia | **B.** tena | **C.** sana | **D.** bado |
| 11. | **A.** kweli | **B.** milele | **C.** kidogo | **D.** kabisa |
| 12. | **A.** ili | **B.** ndio | **C.** ati | **D.** si |
| 13. | **A.** mingine | **B.** vingine | **C.** mengine | **D.** nyingine |
| 14. | **A.** uliendelea | **B.** aliendelea | **C.** iliendelea | **D.** ziliendelea |
| 15. | **A.** kiangazi | **B.** masika | **C.** kipupwe | **D.** upepo |

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Kamilisha sentensi kwa kivumishi kifaacho.
*Basi waliloabiri lilikuwa*
A. bovu. B. libovu.
C. jibovu. D. mbovu.

**17.** Kamilisha sentensi kwa kiashiria sahihi.
*Nitanunua kuku* ________
A. hizi. B. hawa.
C. hivi. D. hii.

**18. Tumia kimilikishi sahihi**
*Leo nimekunywa maji* ________
A. mingi. B. kingi.
C. nyingi. D. mengi.

**19. Kanusha sentensi ifuatayo.**
*Nimechoka sana leo.*
A. Sijachoka sana leo.
B. Sikuchoka sana leo.
C. Sijachoka kidogo leo.
D. Sichoki sana leo.

20. Neno mwembe liko katika ngeli gani?
A. LI - YA B. U - ZI
C. U - I D. YA - YA

21. Akifisha sentensi ifuatayo kwa usahihi.
Je itawezekana
A. Je, itawezekana! B. Je itawesekana?
C. Je, itawezekana? D. Je, itawezekana.

22. Tambua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo?
*Yeye ni mtu mjanja sana.*
A. Mjanja. B. Yeye.
C. Mtu. D. Ni.

23. **Kamilisha sentensi kwa kielezi sahihi**
*Dereva aliegesha gari ________ barabara.*
A. ndani ya B. juu ya
C. katikati ya D. kando ya

24. **Tumia kiunganishi sahihi.**
*Siwezi kula ugali ________ kitoweo.*
A. bila B. wala
C. na D. lakini

25. Ni sentensi ipi ambayo inaonyesha 'ji' ya udogo
A. unanionea kijicho.
B. mtoto amejikata mwenyewe.
C. kijiji hiki kina amani.
D. ameumwa na lile jibwa.

26. Kinyume cha neno 'keti' ni ______.
A. tembea. B. amka.
C. lala. D. simama.

27. Ni maneno gani hayana sauti tatu?
A. Doa, toa. B. Kamba, pamba.
C. Ota, kua. D. Saa, zaa.

28. Ni neno lipi halina uhusiano na mengine?
A. Lima. B. Kilimo.
C. Mkulima. D. Ukulima.

29. **Kamilisha methali ifuatayo**
*Usipoziba ufa utajenga ________.*
A. nyumba. B. ukuta.
C. kibanda. D. kiambaza.

30. Msemo wenye maana 'anza safari' ni_____
A. shika miguu. B. tia nanga.
C. enda mrama. D. shika njia.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31 mpaka 40.***

Pesa ni aina ya sarafu ama noti ambazo hutumika katika shughuli za biashara. Pesa hutumika kununulia ama kulipia bidhaa ama huduma. Pesa zimefanya shughuli za biashara kuwa rahisi sana.

Hapo zamani kabla ya binadamu kugundua matumizi ya pesa walikuwa wakibadilishana bidhaa. Watu walikutana kwenye soko la wazi na bidhaa zao kama vile mikungu ya ndizi, mapakacha ya matunda, vifaa vya kilimo, magunia ya nafaka, mboga, samaki na hata wanyama wa kufugwa. Kila mmoja angebadilishana na mwenzake kulingana na aina na kiasi cha bidhaa ambacho angetaka.

Kazi hii ya kubadilishana ilikuwa ngumu kwa sababu muuzaji na mnunuzi wote walibeba bidhaa. Walibeba bidhaa wakienda sokoni na kubeba nyingine kurudi nazo nyumbani. Lakini sasa mambo ni tofauti. Mnunuzi ndiye anayebeba pesa anapoenda sokoni naye muuzaji hubeba bidhaa. Kisha muuzaji hubeba pesa anapoenda nyumbani naye mnunuzi hubeba bidhaa anaporejea nyumbani. Wakati mwingine muuzaji hurejea na bidhaa kidogo zilizobakia.

Siku hizi pesa zinatumika kila mahali, katika kila nchi na kila mtu. Mbali na kutumika kununulia na kulipia bidhaa zilizotajwa hapo juu, pesa pia hutumika kununulia na kulipia huduma. Mtu anaweza kulipia huduma za stima, maji, elimu, matibabu, usafiri na nyinginezo alizopokea. Watu wanaotoa huduma hizo huwa wamejiajiri au wameajiriwa. Wale walioajiriwa hulipwa mwisho wa siku, juma ama mwezi. Pesa ni nzuri kwa sababu zimefanya maisha kuwa yenye raha zaidi. Ukiwa na pesa unaweza kununua chochote unachotaka ama kwenda popote pale unapotaka duniani.

Ingawa pesa ni nzuri lakini pia hazikosi ubaya wake. Kwa sababu ya tamaa ya pesa watu wengine wameingilia uhalifu. Wametumia njia zisizofaa kama vile wizi na unyang'anyi ili kupata pesa. Hata wengine wamevamia mabenki ili waweze kuzipata kwa urahisi na kwa wingi. Hii imesababisha wao kupoteza maisha kwa kupigwa risasi na polisi ama kufungwa miaka mingi gerezani. Hasara iliyoje! Afadhali mtu afanye kazi kwa mikono yake badala ya kuwa na tamaa. Kumbuka waswahili walisema kuwa tamaa......

31. Pesa zimefanya shughuli za biashara kuwa ________

A. rahisi sana. B. mbaya sana.
C. ngumu sana. D. nzuri sana.

32. Ni gani kati ya pesa hizi za Kenya haina sarafu?

A. Shilingi kumi.
B. Shilingi hamsini.
C. Shilingi ishirini.
D. Shilingi arobaini.

33. Hapo zamani kabla binadamu kugundua matumizi ya pesa walikuwa

A. wakiibiana bidhaa.
B. wakinunuliana bidhaa.
C. wakibadilishana bidhaa.
D. wakiombana bidhaa.

34. Ni bidhaa gani kati ya zile zilizotajwa haziharibiki kwa haraka?

A. Nafaka. B. Ndizi.
C. Matunda. D. Mboga.

35. Kwa nini biashara ya kubadilishana ilikuwa ngumu?

A. Mnunuzi alibeba pesa na muuzaji bidhaa.
B. Muuzaji na mnunuzi walibeba bidhaa.
C. Mununuzi alibeba bidhaa na muuzaji pesa.
D. Mnunuzi na muuzaji walibeba pesa.

36. Wakati mwingine muuzaji hurejea na bidhaa kidogo

A. zilizoharibika. B. zilizoibwa.
C. zilizosahauliwa. D. zilizobakia.

37. Ni kauli gani kati ya hizi si ya kweli? Siku hizi ____________

A. pesa zinatumika kila mahali.
B. pesa zinatengenezwa na kila mtu.
C. pesa zinatumika na kila mtu.
D. pesa zinatumika katika kila nchi.

38. Watu walioajiriwa hulipwa kama ifuatavyo isipokuwa __________

A. mwisho wa siku.
B. mwisho wa juma.
C. mwisho wa mwaka.
D. mwisho wa mwezi.

39. Ni njia gani ya kupata pesa isiyofaa?

A. Unyang'anyi. B. Ukulima.
C. Ufugaji. D. Uvuvi.

40. Kamilisha msemo

Waswahili walisema kuwa tamaa ______

A. iliua mwizi.
B. iliua sungura.
C. iliua mwenye tamaa.
D. iliua fisi.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50.***

Siku moja Kasisi Onesmas alizuru kambi ya chifu ya kona mbaya. Nia yake ilikuwa ni kuwapongeza askari wa chifu kwa kazi nzuri ya kuweka usalama kijijini kona mbaya.

"Hujambo afande?" Kasisi Onesmas alimwamkua mkubwa wa askari katika kambi hiyo.

"Sijambo kasisi Onesmas," askari huyo alijibu huku akishangaa kumwona Kasisi kambini mwa chifu. Alidhani kuwa alikuwa ameleta mashtaka lakini alikosea.

"Nimeonelea nije niwasalimie leo, niwapongeze kwa kazi nzuri na kisha niwanunulie chakula cha mchana kama ishara ya shukrani zangu."

Mkubwa wa askari pamoja na askari wenzake walishangaa sana. Walikuwa hawajawahi kupokea pongezi kutoka kwa mtu yeyote. Walikuwa wamezoea kulaumiwa na kukashifiwa.

Waliondoka, mkubwa wa askari na wenzake watatu waliokuwa chini yake. Walielekea karibu na mkahawa uliokuwa kama hatua ishirini kutoka kambini. Kabla hawajaingia kwenye mkahawa kula chakula, kasisi Onesmas aliwaambia kuwa angependa kwanza kwenda kuwaonyesha nyumba ya mhalifu hatari kijiji humu. Askari hao walitayarisha bunduki zao tayari kwa mapambano.

Kasisi Onesmas aliwapeleka hadi katika nyumba ya akina Matata. Matata alikuwa kijana wa mtaa kwa jina mashuhuri chokoraa. Kijana huyu alikuwa akiwasumbua sana wakazi wa kona mbaya kwa uhalifu mdogomdogo kama vile unyakuzi wa simu na wizi wa vibeti vya akina mama. Mara nyingi askari wa chifu

walimkamata na kumwachilia baada ya kumchapa viboko na kumwonya tu; kwani alionekana kama ***chakaramu***. Mara hii alikuwa korokoroni tena na chifu alikuwa ameamua kumpeleka kituo cha polisi ili apelekwe mahakamani.

Walipoingia nyumbani mwa akina Matata walimpata mama yake akiwa taabani. Alikuwa amekonda kwa sababu ya kuugua kwa muda mrefu kutokana na ukimwi. Askari hao walimsikitikia sana. Walitaka kujua vile alivyojisaidia kwa upande wa chakula na kodi. Mama huyo aliwaeleza kuwa mume wake alikuwa amekufa na kuwa walisaidiwa na mchungaji Onesmas na mtoto wake wa pekee Matata.

"Matata?" Askari hao waliuliza kwa mshangao. "Naam, huyo Matata ambaye mmemsika na sasa mnataka kumpeleka mahakamani akafungwe. Baba yake alifariki akiwa kidato cha tatu, ikabidi aache shule ili aweze kunitunza," mama akaeleza.

Askari hao walishikwa na masikitiko na huruma nyingi. Mkubwa wa askari hao aliamuru kila mmoja achange shilingi mia tano ili mama yake Matata apate chakula. Vilevile aliamuru Matata akaachiliwe na kuahidi kuwa atamrudisha shule aendelee na masomo. Kwa ushirikiano na mbunge wa eneo hilo waliamua kumweka kwenye mpango wa karo ujulikanao kama C.D.F kweli tukijitolea na kuwajibika tunaweza kuleta suluhu kwa matatizo mengi ya kijamii.

---

**41.** Kasisi Onesmas alizuru kambi ya chifu kwa nia ya ____________
- A. kuwapelekea mashtaka.
- B. kuwapa usalama.
- C. kuwapongeza askari.
- D. kujisalimisha kwao.

**42.** Mkubwa wa askari alidhani kuwa Kasisi Onesmas alienda kambini kufanya nini?
- A. Kuwahubiria askari.
- B. Kupeleka mashtaka.
- C. Kuwashambulia askari.
- D. Kuwahubiria waliokamatwa.

**43.** Ni jambo gani si la kweli kuhusu askari wa chifu wa kona mbaya?
- A. Walikuwa hawajawahi kupokea pongezi.
- B. Walikuwa wamezoea kulaumiwa.
- C. Walikuwa wamezoea kusifiwa.
- D. Walikuwa wamezoea kukashifiwa.

**44.** Kasisi Onesmas alipowaambia askari kuwa angewaonyesha nyumba ya mhalifu hatari
- A. walitimua mbio na kurudi kambini.
- B. walimkamata kasisi na kumfungia.
- C. Walikataa kwenda nate wakihofia maisha yao.
- D. Walitayarisha bunduki tayari kwa mapambano.

**45.** Matata alikuwa nani?

| | |
|---|---|
| A. Askari. | B. Chokoraa. |
| C. Kasisi. | D. Jambazi. |

**46.** Neno chakaramu limepigwa stari. Ni neno gani ningefaa kutumika badala yake?
- A. Mwendawazimu.
- B. Mwungwana.
- C. Mstaarabu.
- D. Mpumbavu.

**47.** Mama yake Matata alikuwa akiugua ugonjwa gani?

| | |
|---|---|
| A. Kipindupindu. | B. Ukimwi. |
| C. Kifua kikuu. | D. Malaria. |

**48.** Mwanamke ambaye mume wake amefariki ni __________

| | |
|---|---|
| A. yatima. | B. maskini. |
| C. hayati | D. mjane. |

**49.** Kwa nini mkubwa wa askari aliamuru kila mmoja achange shilingi mia tano?
- A. Ili wale chakula cha mchana.
- B. Ili mama yake Matata apate chakula.
- C. Ili Matata alipiwe karo.
- D. Ili Matata anunuliwe chakula.

**50.** Tunaweza kufunza mambo matatu kutokana na hadithi hii isipokuwa
- A. Hata polisi wana huruma.
- B. Si watu wote hufanya uhalifu kwa kupenda.
- C. Chokoraa wote ni wahalifu wa hiari.
- D. Tukishirikiana tutabadilisha jamii.